# Masahihisho na Vipawa Katika Korintho

## Sura ya 1

**Somo la Kusikiza: Agano jipya #44**

Shabaha: Kuleta utangulizi na picha ya jumla ya barua ya kwanza ya Paulo kwa Wakorintho na kuelewa mada zake muhimu.

*Hata hamkupungukiwa na karama yoyote, mkikutazamia sana kufunuliwa kwake Bwana wetu Yesu Kristo. Mungu ni mwaminifu ambaye mliitwa na yeye mwiingie katika ushirika wa Mwanawe, Yesu Kristo Bwana wetu. Basi ndugu, nawasihi, kwa jina la Bwana wetu Yesu Kristo, kwamba nyote mnene mamoja; wala pasiwe kwenu faraka, bali mhitimu katika nia moja na shauri moja.*

\- 1 Wakorintho 1:7-10

Barua ya kwanza Paulo aliwaandikia Wakorintho ni mfano wa barua za kibinafsi Paulo aliandikia makanisa aliyoanzisha wakati wa huduma yake. Kama zilivyo barua zake nyingi za upuzio, Barua ya kwanza ya Paulo kwa Wakorintho iliandiwa kwa kanisa analolijua vizuri sana, ili aweza kusahihisha makosa na kuagiza na kuhimiza waumini katika imani yao na yetu.

Sura za kwanza kumi na moja za 1 Wakorintho zinaangazia matatizo maalum ambayo Paulo alielewa yalikuwa yanaleta uchungu kanisani. Haya yalikuwa yanazuia kukua kwao kiroho na ushuhuda wao, wa kibinafsi na wa kanisa nzima katika mji wa Korintho. Sura nne za mwisho ni sehemu ya kujenga ya barua hii inayotoa suluhisho kwa shida za kanisa. Kwa kuchunguza shida hizi na suluhisho ambalo Paulo alielezea, tunaweza pata mtazamo wa undani wa namna ya kushughulikia shida hizo hizo zinapotokezea makanisani mwetu leo.

1. Ukweli au **uongo**? Wakati Paulo anapoandikia Wakorintho, alikuwa anaandikia kanisa ambalo hajawahi litembelea.

2. Ukweli au **uongo**? Kanisa la Korintho lilikuwa moja ya yale makanisa machache katika Agano Jipya ambayo yalikuwa hayana shida kabisa ndani yake.

3. **Ukweli** au uongo? Barua ya kwanza ya Paulo kwa Wakorintho ina mambo mengi ya kichungaji na mawaidha ndani yake.

4. **Ukweli** au uongo? Aina ya shida tulizonazo kanisani leo mara nyingi si tofauti na aina ya shida zilizokuwa kwa kanisa la Wakorintho.

***Ikiwa hujaambiwa lingine la kufanya, basi, chagua jibu moja tu kwa kila swali lifuatalo.***

5. Wakorintho lilikuwa kanisa la aina gani ya jumuia?
   a. Kikundi kidogo cha waumini waliokuwa wanapeleleza injili
   **b. Waumini waliokutana kila mara kwa nyumba fulani**
   c. Kusanyiko kubwa kwa jumba kubwa
   d. Shirika la mahali fulani na uongozi wa nguvu wa vyeo kutoka juu

6. Paulo alijuaje kuhusu matatizo ya Kanisa la Wakorintho?
   a. Alipenda kusikia masengenyo kila mara watu walipomwambia
   b. Roho Mtakatifu alimwonyesha katika maono
   **c. Watu kutoka kwa kanisa la Wakorintho walishiriki masikitiko yao na yeye**
   d. Alijionea mwenyewe kwa sababu aliishi Korintho

7. Inamaanisha nini kuwa "aliye takasika" – neno alilotumia Paulo akiwazungumzia Wakorintho?
   a. Kuwa asiye na dhambi na mkamilivu
   b. Kuwa wa kiroho sana kuliko watu wa wastani
   **c. Kutengwa kwa ajili ya kazi maalum ya Mungu**
   d. Kupitia desturi zote za kuongoka

8. Wakorintho walikuwa na shida gani? *(Chagua yote yaliyosahihi)*
   **a. Walikuwa wamegawanyika katika makundi**
   b. Walikuwa na wachungaji wengi kupita kiasi
   c. Walikuwa maskini sana
   **d. Wengine wao walikuwa na tabia mbaya za hadharani**
   e. Walikuwa wakali sana kwa makabiliano na dhambi
   **f. Walikuwa na mafarakano ya kisheria kati yao wenyewe**
   **g. Walitumia vibaya meza ya Bwana**
   h. Walikuwa watu wa kawaida sana kudai kuwa walikuwa na vipawa vyovyote
   **i. Walijivunia vipawa vya kiroho na wakavitumia vibaya**

9. Ni nia gani ambayo Paulo alisema kuwa ni ya muhimu zaidi kuliko zote katika utendaji kazi wa karama za kiroho?

a. Juhudi
**b. Upendo**
c. Nidhamu
d. Kutaka makuu

10. Kulingana na Paulo, ni nguvu gani zinazoweza kusuluhisha shida kanisani?

**a. Nguvu zilizo mfufua Yesu, zinazo tuwezesha kuishi katika njia mpya**
b. Nguvu za kufikiria mazuri pekee
c. Nguvu za sheria ambayo Mungu alitupa katika Agano la Kale
d. Nguvu za kisheria za serikali ya mitaa

Kati ya shida za kiroho za Wakorintho, ni gani ambayo wewe unaweza husiana nayo? Ni vipi uhusiano wetu na Yesu na nguvu zake za ufufuo vinaweza kutuzaidia kushinda shida hizo?

_____

_____

_____

Mshukuru Mungu kwamba Roho wake ametupa majibu ya nguvu na ya vitendo kuelekea mahitaji ya ndani zaidi ya mioyo yetu. Muulize akujaze na upendo wake na nguvu za ufufuo unapoendelea kumtumainia na kutafuta kumfuata kila mara. Omba kuwa atabariki kujifunza kwako Neno Lake unapojifunza zaidi Wakorintho 1 na 2.

**KUZAMA ZAIDI**

1. Elezea na kutia katika matumizi namna ambayo upuzio wa suluhisho maalum kwa matatizo haya katika Kanisa la Wakorintho kutoka kwa Paulo, unatupa upuzio wa kipeo cha kutumia kama Mwongozo wa Uchungaji, tunaposhughulikia matatizo hayo makanisani mwetu leo.

_____

_____

2. Kuongezea kwa suluhisho hizi maalum kwa shida za binafsi, elezea na kutia katika matumizi vile upendo kama ulivyoelezewa katika sura ya 13, ni suluhisho la jumla kwa shida hizi zote.

_____

_____

3. Fafanua na kutia kwa matumizi kile ambacho Paulo alimaanisha alipoweka shida hizi zote kwa kundi la vitu vya kimwili katika kanisa la Korintho, katika sura 12, anatangaza kuwa hatimaye ataenda kujadiliana nao mambo ya kiroho kanisani. _____

_____

_____

4. Elezea na kutia katika matumizi mambo ya kiroho anayoshughulikia katika barua hii kuwa yote ni sehemu ya upuzio wa suluhisho la jumla analoelezea kanisa hili katika upuzio wa barua hii ya masahihisho. _____

_____

_____

5. Elezea na kutia katika matumizi jinsi nguvu za ufufuo zinavyokuwa sehemu ya suluhisho la jumla kwa shida hizi zote maalum. _____

_____

_____

6. Baada ya kutuinua hadi kimo cha ufasaha wa usemi katika majadiliano ya ufufuo kwa sura ya 15, Je, anabadilisha somo ghafla au anatufahamisha kitu kingine cha kiroho wakati anapoandika, “Kwa habari ya ile changizo” kwa aya ya kwanza ya sura 16? Elezea. _____

_____

_____

7. Elezea na kutia kwa matumizi laini ya chini kabisa ya suluhisho mwafaka kwa shida ya ndugu dhaifu kiimani na jambo la kula vitu vilivyotolewa kama dhabihu kwa sanamu za mashetani kama ilivyojadiliwa katika sura ya 8-11. _____

_____